

HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA.

SHULE YA SEKONDARI RAFSANJANI SOGA,
S.L.P 30288,
KIBAHA – PWANI
SIMU: 0786 313 310
0713039946

18/5/2018.

KUMB NA. RAFSS/J.1/F.5/2018

MWANAFUNZI.....
S.L.P
.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE.

1.0. UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Rafsanjani – Soga mwaka **2018/ 2019** Tahasusi/Combination ya Unapaswa kufika shuleni tarehe Kabla ya saa 11 Jioni.

1.1. JINSI YA KUFIKA SHULENI.

Shule ipo kata ya Soga, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Mkoa wa Pwani Ukitoka Morogoro au Dar es Salaam utashuka kituo cha basi Kongowe (Kibaha) utaona kibao cha shule ya Sekondari Rafsanjani Soga. Usafiri wa kufika shuleni utapatikana nauli ni Tshs 1,000/= kwa gari na 2,000/= kwa pikipiki.

2.0. ADA NA MICHANGO YA SHULE

S/N	MICHANGO	KIASI Tshs
1.	Ada ya shule	70,000.00 kwa mwaka 35,000.00 kwa muhula
2.	Taaluma	20,000.00 kwa mwaka
3.	Tahadhari	5,000.00(haitarejeshwa)
4.	Mpishi na ulinzi	30,000.00 kwa mwaka
5.	Matibabu (huduma ya kwanza)	10,000.00 kwa mwaka
6.	Ukarabati wa samani	15,000.00 Mara moja
JUMLA KUU NI Tshs		150,000.00

Fedha hizi zilipwe kwenye akaunti ya shule ya NMB, 21203500177, RAFSANJANI SOGA SECONDARY SCHOOL, kisha mwanafunzi aje na stakabadhi ya malipo (Bank pay in slip) ikionyesha jina kamili la Mwanafunzi na kidato siku anaporipoti shuleni.

3.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

3.1. SARE YA SHULE

- a) Sketi mbili (2) za rangi ya bluu bahari (Light blue kitambaa kimeambatanishwa) mshono wa sketi ni rinda moja mbele mfano wa V – yenye urefu wa kuvuka magoti na isiyobana.
- b) Mashati meupe (Tomato) ya mikono mifupi mawili (2)
- c) Soksi nyeupe jozi mbili (2)
- d) Sweta yenye shingo V ya rangi ya udongo (Brown) kwa wanaohitaji
- e) Skafu ya light blue
- f) Viatu vyeusi vya kufunika jozi mbili visiwe na urembo
- g) Truck suit ya rangi ya bluu bahari isiyobana kwa ajili ya kuvaa usiku wakatio wa kujisomea (Preparation).

NB: Kwa waumini wa dini ya Kiislam wanaopenda kuvaa hijabu wanaruhusiwa kwa kuzingatia mshono na rangi zilizotajwa hapo juu.

3.2. MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

- (a) Bunda (Ream) ya karatasi 1 kwa mwaka
- (b) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Orodha imeambatanishwa)
- (c) Sare ya mchezo Bukta rangi ya bluu moja (1) na Raba jozi moja (1)
- (d) Shuka nne (4) za rangi ya pinki
- (e) Godoro linakodishwa shuleni kwa Tshs 10,000.00 kwa mwaka.
- (f) Mto na foronya
- (g) Chandarua ya kuzuia mbu rangi nyeupe.
- (h) Ndoo mbili (2) ndogo zenye mifuniko
- (i) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe, kijiko na chupa ya chai ndogo)
- (j) Tochi ya betri au taa ya solar kwa tahadhari ya umeme ukikatika.
- (k) Madaftari makubwa (counter book) sita (6)
- (l) Scientific calculator (kwa wanafunzi wa Sayansi)
- (m) Kitambulisho cha bima ya afya kama anacho

- (n) Nakala ya hati ya cheti cha kuzaliwa
- (o) Hati ya matokeo ya kidato cha nne
- (p) Koti (lab coat) nyeupe kwa matumizi ya maabara masomo ya Sayansi.
- (q) Fomu ya maelezo ya Daktari kuhusu afya yako ikiwa imejazwa (imeambatanishwa)
- (r) Sheria za shule zimeambatanishwa- hakikisha umezisoma na kuzielewa
- (s) Vifaa vya usafi (kwanja, jembe, reki, mifagio ya ndani na nje) unapaswa kuleta shuleni (i) (ii) (iii).....

4.0. MENGINEYO

- (a) Mwanafunzi aje na fedha taslimu sh 10,000.00 ya fulana moja (1)
- (b) Picha na kitambulisho shs. 6,000.00
- (c) Nembo sh. 2000.00
- (d) Sanduka la bati (tranka) moja.
- (e) Ni jukumu la mzazi/mlezi kugharamia usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani pia kumpatia mwanafunzi fedha za kutosha za matumizi binafsi awapo shuleni.
- (f) Nguo za nyumbani haziruhusiwi. Mwanafunzi aje na sketi mbili nyeusi au zaidi za kushindia. Vifaa binafsi kama taulo, kandambili, nguo za ndani, kanga/kitenge n.k. haturuhusu kusuka nywele.

Nakutakia maandalizi mema.

Karibu sana Rafsanjani Soga Sekondari.

**CHIMAZI J.C
MKUU WA SHULE**